# ***TIBA NA KINGA DHIDI YA MAGOJWA YA KUKU***

## UTANGULIZI

# Magonjwa na ufugaji wa kuku



- Nini tofauti ya tiba na chanjo na kinga



- Ugonjwa husababishwa na nini?
    - Virusi,
    - Bacteria,

– Protozoa,

– Upungufu wa viini lishe

# MDONDO



# MDONDO

- Mdondo Kuku wote yaani wakubwa na wadogo huweza kuugua na kufa kwa mdondo. Husababishwa na virusi.

Dalili za mdondo.

- Kuku kuacha kula, kuharisha, kutoa machozi na kamasi pia kupumua kwa shida. Baadhi hupooza au kuzungusha kichwa na kutembea kinyume nyume.

Tiba na kinga

- Ugonjwa hauna dawa ya kutibu, lakini unaweza kukingwa kwa chanjo. Chanjo itolewe kila baada ya miezi mitatu.




# Gumboro

- Ni ugonjwa hatari unaosababishwa na virus,
- Virus husambazwa kutoka kwa kuku aliyeathrika kupitia kinyesi

- Ni kirusi mgumu sana kuondolewa kwenye mazingira

Dalili.

- maambukizi yanategemea umri na kuku na aina ya kirusi
- Dalili huanza kuonekana kuanzia wiki ya sita hadi 18
- Kuku kuharisha maji maji

- Maambukizi yanaweza kufikia 100%, na vifo 5%–20%.

- Afya huanza kuimarika <1 wk

Kinga

Hakuna tiba, chanjo



# Ndui ya kuku



- Ndui ya kuku, Ndui husababishwa na virusi na huathiri sana vifaranga wanaokua na hujitokeza zaidi wakati wa mvua.

*Dalili za ndui ya kuku*

- Husababisha vivimbe katika kichwa uso, kishungi na hata sehemu zinazozunguka macho na mdomo.

Tiba na Kinga

- Dawa za kuua vimelea kama ‘joto ya vidonda’ hupunguza makali ya madonda.

- Chanjo ya sindano itolewe kabla ya msimu wa mvua ndefu kuanza.







# UPUNGUFU WA VITAMINI A



- Ukosefu wa vitamini‘A’ Hujitokeza baada ya kuku kukosa vyakula vyenye vitamin ‘A’ kwa muda mrefu.
  – Kuku wadogo huathirika zaidi kwa ukosefu wa vitamini ‘A’.

Dalili za ukosefu wa vitamini ‘A’

- Macho huvimba na kutoa uchafu mzito kama sabuni ya mche iliyolowana maji.
- Hudhoofika na hatimaye hufa.

Tiba na Kinga.

- Hakuna tiba mara ugonjwa ukianza kujitokeza.

- Kinga ugonjwa huu kwa kuwapa majani mabichi au mchicha wakati wa kiangazi.
- Wape kuku vitamini za kuku za dukani wakati majani hayapatikani.



# KOKSIDIOSISI

- Koksidiosisi, Koksidiosisi ni ugonjwa wa vimelea huathiri zaidi na kuua kuku wadogo kuanzia umri wa wiki moja.

Dalili za koksidiosisi

- Kuku hudhoofika, manyoya huvurugika na kuku kuzubaa na kuwa kama amevaa koti.
- Kinyesi huwa na rangi ya kahawia au chenye damu.

**Tiba na Kinga.**

- Koksidiosisi hutibiwa kwa dawa maalumu kama

‘Amprolium’ au ‘Sulfa’.

- Dawa hizi pia huzuia kujitokeza kwa ugonjwa zikitumiwa ipasavyo

# KOKSIDIOSISI




Kinyensi huwa na rangi ya kahawia au chenye Damu.




# Minyoo Michango

- Hukaa tumboni.
- Kupunguza kutaga.
- Kuharisha.
- Kupoteza uzito.



# Michango ya tumboni



Tiba

- Piperazine

# VIROBOTO UTITIRI

- Viroboto na utitiri Viroboto hushambulia kichwa na kunata huku vikinyonya damu. Viroboto huua zaidi vifaranga.  Chawa na utitiri hughasi hata tetea wakashindwa kutaga na kuatamia.



Tiba na Kinga

- Tumia dawa za kuua wadudu kama 'Akheri powder' au 'Sevin dust'. Wamwagie kuku dawa pia na malazi yao ili kuua wadudu wote.

- PROMECTIN- ORAL 100ml
- 1.5cc in 1 litre

| UGONJWA | UTARATIBU WA KINGA |
| --- | --- |
| Mdondo | Kuku wote wachanjwe kila baada ya miezi mitatu. |
| Ndui | Chanjo ni ya sindano itolewe na mtaalamu kabla ya mvua ndefu kuanza. |
| Ukosefu wa vitamini ‘A’ | Wapatie kuku majani mabichi au mchicha mara kwa mara. Kama hakuna majani wape vitamini za kuku toka duka la dawa za mifugo katika pumba au maji ya kunywa kama utakavyoshauriwa na mtaalamu. |
| Koksidiosisi | Safisha banda kila siku na hakikisha hakuna unyevu sakafuni. Wapatie kuku dawa za kinga kama ‘Amprolium’ au ‘sulfa’ kwa siku 3 mfululizo mara wafikishapo umri wa siku 7. |
| Viroboto,chawa utitiri | Mwagia majivu katika banda na hasa viota vya kutagia ili kukinga wadudu. Tumia dawa za dukani mfano ‘AKHERI POWDER’ na ‘SEVIN DUST’kumwagia kuku mwilini na |

| | |
|---|---|
| | katika mazingira. Paka mafuta ya taa kwa kutumia unyoya wa kuku kwenye viroboto vinavyoonekana. |
| | |

**KWA MAHITAJI YA YA HUDUMA ZIFUATAZO**

- ✓ Vifaranga siku,wiki na mwezi aina zote
    - ✓ Mayai ya kuku ya kutotoleasha aina ya SASSO na KROILER
    - ✓ Usimamizi wa mradi wa ufugaji kuku

- ✓ Ushauri Zaidi juu ya ufugaji
- ✓ Uandishi wa mchanganuo biashara ya ufugaji
- ✓ Utafutaji wa masoko ya ufugaji.

**WASILIANA NAMI KWA**

NAMBA ZA SIMU: 06564469991 Tigo
0620765518 Halotel
BARUA PEPE : Godwinmbwambo111